TANGAZO LA SERIKALI NA.....LA TAREHE .....

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288 YA 2002)
SHERIA NDOGO
Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (KILIMO, NA USALAMA WA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA, 2017

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kilimo, Umwagiliaji na Usalama wa Chakula) za Halmashauri ya Manispaa ya Musoma za mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. — Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. — Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo:- — Fafsiri

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Afisa Ugani" maana yake ni mtaalamu wa kilimo katika ngazi za kata au mtaa.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma

"Kilimo" maana yake ni shughuli yoyote ya uzalishaji mali inayofanywa na binadamu na itajumuisha kilimo cha mazao ya chakula, biashara, mboga mboga, miti ya matunda, miti ya mapambo na maua.

"Mazao ya chakula " maana yake ni mazao ambayo hutumika kwa chakula cha binadamu.

"Wanyama na wadudu waharibifu" maana yake ni wanyama au wadudu ambao uharibu mazao au mimea ya chakula ikiwa shambani au ghalani.

"Maji ya asili" maana yake ni maji ya ziwa, mito na visima vya asili ambayo hutumika kwa shughuli za kilimo.

4. (1). Katika kuhamasisha na kutekeleza azma ya Kilimo bora, Halmashauri kupitia wataalam wake itakuwa na wajibu wa;- — Wajibu wa Halmashauri kutekeleza majukumu ya usimamizi wa

(a) kuhakikisha kuwa wakulima wanasajiliwa pamoja na mazao wanayolima na

kiasi cha ekari ya mazao wanayolima

kilimo na mazao

(b) kuhakikisha wakulima waliosajiliwa wanashiriki ipasavyo katika kuendeleza sekta ya kilimo katika Halmashauri;

c) kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani katika kila Kata;

(c) kusimamia upatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine za kilimo;

(d) kuhakikisha ubora wa mazao unazingatiwa na mkulima katika hatua zote za uzalishaji.

(e) kuhakikisha visumbufu na magonjwa ya mazao yanadhibitiwa

(f) kuhakikisha kuwa mazao yanayolimwa si yale yanayorefuka na kusababisha giza.

(g) kuhakikisha kunakuwa na masoko rasmi yanayotambulika.

5. Katika kuhamasisha na kutekeleza azma ya Kilimo bora cha mazao Halmashauri itakuwa na wajibu wa;-

(a) kuhamasisha uandaaji wa vikundi vya kiuchumi vitakavyotekeleza kilimo bora kinachofaa katika maeneo ndani ya Halmashauri .
(b) kuweka kwenye mbao za matangazo kwa kila kata maelezo yanayoelekeza kanuni bora za kilimo yanayopaswa kuzingatiwa na mkulima kwa mazao yanayolimwa kwenye eneo hilo.

(c) kuanzisha mashamba darasa ya mfano katika kila kata

(d) kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya wakulima vya kuweka na kukopa kwa lengo la kujipatia mitaji yenye riba nafuu .

(e) kushindanisha wakulima pia maafisa ugani katika kata na mitaa ili kupata mkulima bora, Afisa Ugani bora katika Halmashauri, Kata, mtaa.

(f) Kuhamasisha wananchi kujinunulia na kutunza chakula wakati wa msimu wa mavuno.

(g) Halmashauri kushirikiana na vituo na taasisi za utafiti katika utafiti wa mazao.

6. (1). Serikali ya mtaa itakuwa na wajibu ufuatao;

Wajibu wa Serikali ya Mtaa kutekeleza

(a) Kusajili wakulima, eneo na mazao wanayolima

(b) Kuhakikisha kuwa sheria za mazao na kanuni zake zinatekelezwa

majukumu ya usimamizi

7. (1). Afisa mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mkulima;-

Wajibu wa Afisa muidhiniwa

(a) anaandaa shamba kwa wakati;

(b) anapanda mbegu kwa mstari;

(c) anazingatia nafasi kati ya mmea na mmea inayotakiwa kitaalamu;

(d) anaweka mbolea kwa viwango na kwa wakati;

(e) anapalilia kwa wakati

(2). Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia na kukagua shamba lolote wakati wa saa za kazi ili kujionea kama mkulima amezingatia maelezo ya kitaalamu kama yalivyotolewa na watalamu wa kilimo,

8. (1) Itakuwa ni jukumu la kila mkazi hususani mkuu wa kaya kuhakikisha kuwa anahifadhi chakula cha kutosha yeye na familia yake kwa angalau mwaka mmoja au zaidi.

Hifadhi ya mazao

9. Kila mkazi anayelima katika eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma atahitajika kutekeleza kanuni bora za kilimo kama zilivyoainishwa katika ibara ya 4, kifungu cha 1 (a) – (e).

Wajibu wa mkulima

(1). Bila kuathiri kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi itakuwa ni wajibu wa kila Mkulima:-

(a) kutoa taarifa kwa Afisa Ugani wa kata yake kwa njia yoyote atakayoona inafaa kuhusu kuwepo kwa ugonjwa wa mazao au kuwepo kwa wadudu waharibifu;
(b) kutumia pembejeo kwa kuzingatia maelezo ya kitaalamu kila mwaka isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Afisa Ugani;
(c) kuchukua hatua za kuangamiza wadudu waharibifu au kutibu magonjwa kama atakavyokuwa ameelekezwa na Afisa Ugani

(2). Kila Afisa Ugani atawajibika kutoa programu ya kilimo ya mwaka kulingana na hali ya hewa, ambayo itazingatia mambo yafuayato:

(a) aina ya mazao kwa msimu;
(b) aina ya mbegu kwa msimu husika;
(c) namna na wakati wa kupanda;
(d) namna na wakati gani wa kuvuna;
(e) namna ya kuhifadhi mazao baada ya kuvunwa.

10. Afisa mwidhiniwa akishirikiana na Afisa Ugani, wakati wowote wa saa za

kazi; Ukaguzi

(a) ataweza wakati wowote wa saa za kazi kuingia kwenye eneo la kilimo kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
(b) ataweza kuingia katika kaya yoyote ili kukagua ili kujua kama taratibu za kuhifadhi chakula zinazingatiwa;

(c) ataweza kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi;

(d) atatakiwa kuwa na daftari linaloonyesha idadi kamili ya wakazi na idadi ya ekari za mazao ya kilimo;

(e) atapanga ratiba ya kutembelea mashamba ya wakazi ili kujionea kama wanatekeleza wajibu wa kulima na kutunza mashamba kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

Kila Afisa Mtendaji wa kata au mtaa atawajibika kutunza kumbukumbu za wakulima katika Kata au mtaa wake na atasimamia moja kwa moja utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

11. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote; Makosa

(a) kutotunza shamba na mazao yaliyolimwa kwa msimu husika;
(b) kutovuna kwa wakati mazao yaliyoko shambani ambayo yamefikia wakati wa kuvunwa;
(c) kuuza mazao yakiwa shambani;
(d) kutumia hifadhi ya mazao kwa ajili ya kutengenezea pombe,
(e) Kulima mazao bila kufuata kanuni bora za kilimo.

12. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na sheria ndogo hizi atashtakiwa, akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki moja (200,000) na isiyozidi million moja au kwenda jela kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja Adhabu

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kilichofanyika tarehe ……mwezi ……mwaka 2017 mbele ya:

……..
MH: PATRICK WILLIUM GUMBO
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA

…….
FIDELICA G. MYOVELLA
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA

NAKUBALI,

TAREHE …..... ……
DODOMA **MH. GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)**
WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI